**JESMA 005**

# JARIBIO LA TANO K.C.P.E
# DARASA LA NANE

**KISWAHILI**
**SEHEMU YA KWANZA: LUGHA**

**Muda: Saa 1 dakika 40**

**SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

**NAMBA YAKO YA MTIHANI**
**JINA LAKO**
**JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule. Na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu.
9. Kwa kila swali 1 – 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C na D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambayo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano**

**Katika kijitabu cha maswali:**

**11.** Mtu anayetengeneza vyombo vya vyuma ni
A. sonara
B. rubani
C. mhunzi
D. mwashi

Jibu sahihi ni C

**1** [A] [B] [C] [D] **11** [A] [B] [▬] [D] **21** [A] [B] [C] [D] **31** [A] [B] [C] [D] **41** [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 11, kisanduku chenye herufi C ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kitabu hiki cha maswali kina kurasa 8 zilizopigwa chapa**

**Watahiniwa ni lazima wahakikishe kuwa kurasa zote za karatasi ya mtihani zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**

*Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.*

Bwana Hamisi ni seremala ____1____ sana katika mtaa wetu. Ana ____2____ kubwa ambapo yeye huundia samani maridadi sana. Ufikapo hapo, hutakosa kuviona vifaa mbalimbali, kama vile ____3____, anavyotumia katika kazi yake. ____4____ vijana wengi wanaokosa karo humwendea kwa mafunzo ili waweze kujitegemea baadaye. Yeye pia ana ____5____ maadamu huwapa vijana hawa ujira kila jioni ili nao wajiendeshee maisha yao. Sifa zake ____6____ kote mtaani. Hupenda kusema kuwa siri ya maisha ni bidii huku akihimiza kuwa ____7____. Vijulanga ____8____ na uhaba wa kazi ____9____ nchini hawana budi kuiga mfano wake.

**1.** A. hatari B. maalum C. mahiri D. marufuku

**2.** A. karakana B. kiwanda C. maabara D. ofisi

**3.** A. kekee, fuawe, kombeo na pimamaji B. utepe bisibisi, jiriwa na patasi C. vipuli, mvukuto, timazi na nyundo D. msumeno, kekee, chelezo na mvuo

**4.** A. Kwani B. Lakini C. Ijapokuwa D. Aghalabu

**5.** A. mkono wazi B. mkono birika C. mkono mzuri D. mkono mwepesi

**6.** A. zimesambaratika B. zimetanda C. zimesheheni D. zimetalii

**7.** A. ukipanda upepo utavuna tufani B. bandu bandu humaliza gogo C. cha kuzama hakina rubani D. mgaagaa na upwa haondoki patupu

**8.** A. walioadhirika B. walioathiriwa C. walioadhiriwa D. walioathirika

**9.** A. kote B. wote C. zote D. yote

Vita ____10____ mihadarati si vya ____11____ mzaha hata kidogo. Hili ni janga linalotishia kuwasomba vijana kwa mkupuo mmoja. Wakwasi wenye ____12____ wa darahima wanawauzia wana wetu sumu hii bila kujali lolote. Wavyele ambao ____13____ kuwa ____14____ cha kuigwa nao wamejitia hamnazo kucheza ngoma watakazo. Si ajabu kumwona baba au mama akirejea mastakimuni huku amelewa kama ____15____ na kuanza kuwafokea wanawe.

**10.** A. juu ya B. baina ya C. dhidi ya D. kutokana na

**11.** A. kufanya B. kufanyiwa C. kufanyia D. kufanywa

**12.** A. umero B. tamaa C. shauku D. ukata

**13.** A. watatarajwa B. wangetarajiwa C. walitarajiwa D. wanatarajiwa

**14.** A. kielezi B. kielelezo C. chombo D. chelezo

**15.** A. pombe B. mjinga C. komba D. nyani

***Kuanzia swali la 16 mpaka 30, jibu kila swali kulingana na maagizo uliyopewa.***

**16.** Kati ya viteuzi vifuatavyo, kipi kinaonyesha kuendelea kwa kitendo?

A. Jua lachoma vikali leo.
B. Walizioka keki tamu wakaziuza.
C. Ukifanya bidii utapita mtihani.
D. Tulikuwa tukitembea mvua ilipoanza kunyesha.

**17.** Ni orodha gani inayoonyesha vielezi pekee?

A. Mombasa, kesho, vibaya, kila siku.
B. Kwake, zuri, polepole, chochote.
C. Vigumu, baya, kubwa, aghalabu.
D. Baada ya vyote, taratibu, chekesha.

**18.** Mibuni hutupatia kahawa. Je, mibono huzaa nini?

A. Mabono
B. Mbarika
C. Tunguja
D. Kanju

**19.** Tegua kitendawili kifuatacho:

Huwafanya watu walie huku wakicheka.

A. Kifo
B. Pilipili mboga
C. Kiboko
D. Moshi

**20.** Tambulisha sentensi iliyoakifishwa barabara.

A. Ala? Kumbe unaishi katika mji huu!
B. Je? Huu ni uungwana kweli?
C. Nilipofika huko sikumpata; alikuwa amesafiri.
D. Tafadhali niletee, maji, sabuni, dodoki.

**21.** Maelezo yapi hayana maana ya <u>panga</u>?

A. Kaa mahali kwa makubaliano fulani.
B. Chombo cha kuleta baridi kinachozungushwa na umeme
C. Weka vitu kwa utaratibu mzuri.
D. Mahali maalum pa kufanyia matambiko.

**22.** Badili sentensi ifuatayo katika ngeli ya PA-KU-MU.

Shule yao ina wanafunzi wengi.

A. Shule zao zina wanafunzi wengi.
B. Shuleni mwao kuna wanafunzi wengi.
C. Shuleni pao mna wanafunzi wengi.
D. Shuleni mwao mna wanafunzi wengi.

**23.** Upi ni usemi wa taarifu wa senteni hii.

Mama alisema, "Tafadhali niwashie jiko niteleke chungu".

A. Mama alimwomba amwashie jiko ili ateleke chungu.
B. Mama aliagiza awashiwe jiko ili ateleke chungu.
C. Mama alisema angewashiwa jiko angeteleka chungu.
D. Mama alimwambia amwashie jiko wateleke chungu.

**24.** Andika udogo wa:

Mlango mpana umefunguka.

A. Lango pana limefunguka.
B. Jilango pana limefunguka.
C. Kilango kipana kimefunguka.
D. Kijilango kipana kimefunguka.

**25.** Kanusha sentensi ifuatayo kwa usahihi:

Maji yasingepatikana upesi mifugo yetu ingeangamia.

A. Maji yangalipatikana upesi mifuo yetu isingeangamia.
B. Maji yangepatikana upesi mifugo yetu isingeangamia.
C. Maji yasingepatikana upesi mifugo yetu isingeangamia.
D. Maji yangepatikana upesi mifuo yetu ingeangamia.

**26.** "Gao huwa chombo wakatiwe" ni kwa wanaovidharau vitu vikuu; kama vile "ganda la muwa la jana chungu kaona kivuno" ni kwa wale

A. wanaovidharu vitu vidogo.
B. wanaopuuza msaada mkubwa.
C. wanaopuuza mali ya wengine.
D. wanaotamani mali ya wengine.

27. Ugonjwa wa macho unaoweza kusababisha upofu ni
   A. ukoma
   B. machapwi
   C. trakoma
   D. afkani

28. Ni sentensi ipi iliyo na kivumishi cha pekee?
   A. Wazee wengi walitoa michango yao.
   B. Wazee wale walitoa michango yao.
   C. Wazee wenu walitoa michango mizuri.
   D. Wazee wengine walitoa michango mikubwa.

29. Mtu anayeongea kwa ncha ya ulimi huitwa
   A. kithembe
   B. kigugumizi
   C. kiduko
   D. kiduvya

30. Kamilisha kwa ufasaha:

   Mtoto huyu, huyo na yule ______.

   A. mnifuate
   B. wanifuate
   C. anifuate
   D. tufuate

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali* **31 – 40**.

Bwana Aisee aliporejea jijini alifungua ofisi kubwa aliyoipamba kwa samani za hali ya juu. Kisha aliwasiliana na waandishi wa magazeti mbalimbali. Alidai kuwa kulikuwako na mradi kabambe wa kuhakikisha kuwa vijana waliokosa amali wangeajiriwa kazi za maana kwenye hoteli za kitalii huko Uarabuni na Ulaya na hata kwenye meli za kifahari. Viongozi wengi walimshehenezea Bwana Aisee sifa kemkemu, "Huyu ni mzalendo kindakindaki! Anawakumbuka raia wenzake ambao hawana bahati kama yeye!" Vijulanga waliokuwa na hamu na ghamu ya kuenda ugenini walifurika ilipokuwa ofisi yake.

Walichohitajika kufanya tu ni kulipa ada ya shilingi elfu tano pamoja na kiasi kingine kama hicho kugharimia vyeti vya usafiri. Licha ya kuwa wengi wao hawakuwa na namna ya kuzipata pesa hizo, walikuwa radhi kukopa wahakikishe kuwa wamepata nafasi hizo adimu. Vijana hao pia walitakiwa kuenda hospitali fulani ya kibinafsi kufanyiwa uchunguzi wa kimatibabu. "Aisee bwana, huo ndio ustaarabu wa wenzetu walioendelea. Ukitaka kumwajiri mtu lazima uijue siha yake ikoje," Bwana Aisee aliwakumbusha. Hamna aliyejali. Kilichokuwa muhimu ni kuwa, baada ya miezi miwili wangepata kazi ambazo zingewafanya waupige kumbo la milele ukata uliotishia kuwagubika kama wingu.

Baada ya kuzikusanya hela hizo zilizolipwa na vijana zaidi ya elfu thelathini, Bwana Aisee aliwaambia wangoje kwa muda wa miezi miwili. Muda waliokuwa wamepewa wa kungoja mambo yaive ukapita. Tarehe ya kusafiri kuenda kuanza kazi zao ikaahirishwa. Taarifa iliyotoka katika ofisi kuu huko ulaya ilidai kuwa kuahirishwa huko kulitokana na hali mbaya ya usalama. Tarehe hizo zilipokwisha kuahirishwa mara nyingine mbili, kila mmoja alianza kutuhumu kuwa palikuwa na jambo. Malalamishi ya kila aina yalianza kusikika kwenye vyombo vya habari. Wakaanza kumsaka Bwana Aisee. Lakini hawakujua kumbe <u>bwana huyo alikuwa ameingi mitini</u>.

Uchunguzi wa historia ya Bwana Aisee ulianza kufanywa. Jamaa waliosoma naye walitoa habari zake zote bila kusaza lolote. Walieleza jinsi alivyokua fundi wa kuongea kizungu. "Lakini huyu si fundi wa kizungu tu bali na mizungu pia!" Walisema wengine kwa hasira walipozisikia habari hizo. Serikali ilianza mipango kabambe ya kumsaka Bwana Aisee. Ilibidi kuwashirikisha wachunguzi wa polisi wa kimataifa, INTERPOL, katika swala zima. Haikuchukua muda kabla ya kugunduliwa kuwa mashirika yaliyodaiwa kuhusika na suala la ajira hizo yalikuwa bandia.

Mambo yaliendelea kukanganya wakati ofisi ya Bwana Aisee iliyokuwa jijini ilipochomeka siku moja wakati wa usiku na vyeti vyote kuteketea. Nayo hospitali waliyokuwa wameenda kufanyiwa uchunguzi wa kiafya wale walioenda kuomba kazi ilifungwa ghafla na daktari aliyehusika kutoweka. Ilikuwa wazi sasa kuwa watu walikuwa wametapeliwa.

Kashfa hii ilizungumziwa na wengi kote nchini si katika redio wala runinga bali pia magazetini na kwingineko. Adinasi waliapiza. Lakini njia ya mwongo ni fupi. Aisee <u>alibambwa</u> na polisi wa kimataifa alipokuwa katika uwanja wa ndege wa Frankfurt huko Ujerumani akijitayarisha kuabiri ndege kuelekea Afghanistan alikopanga kujificha kwa muda hadi mambo yatulie.

Baada ya kutiwa mikononi, Bwana Aisee alisafirishwa chini ya ulinzi mkali hadi jijini Nairobi alipofikishwa mbele ya hakimu. Kesi yake ilihudhuriwa na mamia ya vijana waliohasirika. Mwishowe Bwana Aisee alitumbukizwa gerezani kwa miaka minane ikiandamana na kazi za sulubu. Mizungu yake ilikuwa imegota mwamba.

**31.** Lengo la Bwana Aisee kuwasiliana na wanahabari lilikuwa
A. kuwafahamisha kuhusu ofisi yake.
B. kuwaeleza kuhusu mradi wake.
C. kutoa tangazo kuhusu mradi wake.
D. kutoa tangazo kuhusu ofisi yake.

**32.** Wengi waliosikia kuhusu mipango ya Bwana Aisee
A. walimsifu kuwa mpenzi kamili wa nchi yake.
B. walimwona kama adui mkubwa wa nchi.
C. walimsifu kwa kuleta mapinduzi nchini.
D. walimshuku kuhusu nia ya kazi yake.

**33.** Ili kusajiliwa kila mhusika alihitaji kulipa shilingi elfu
A. tano, kufanyiwa uchunguzi wa kiafya.
B. kumi, kuchunguzwa afya yake.
C. tano, kuwasilisha vyeti vya usafiri.
D. kumi, vyeti vya usafiri na kuchunguzwa.

**34.** Watu walianza kutuhumu kuwa mambo hayakuwa sawa
A. baada ya tarehe ya kuanza kazi kuahirishwa.
B. tarehe ya kusafiri ilipoahirishwa tena.
C. Bwana Aisee alipotoweka kutoka jijini.
D. tarehe ya usafiri ilipoahirishwa kwa mara ya tatu.

**35.** '.....bwana huyo alikuwa ameingia mitini' maana yake ni kuwa alikuwa
A. ametoweka baada ya kufanya uhalifu.
B. ameshiriki uhalifu wa kuibia umma.
C. ameshapatwa na mabaya.
D. amejitia katika mambo asiyoyafahamu.

**36.** Historia ya Bwana Aisee ilibainisha kuwa alikuwa na hulka ya
A. kuwaibia watu
B. kusema kimombo
C. kusafiri uarabuni
D. kuwapenda watu

**37.** Inaonekana kuwa asili ya kuchomeka kwa ofisi ya Bwana Aisee ilikuwa
A. kuficha historia yake.
B. hasira za vijana walioibiwa.
C. kuharibu ushahidi dhidi yake.
D. harakati za polisi wa INTERPOL.

**38.** Badala ya kusema alibambwa, pia tunaweza kusema
A. alibakwa
B. alinaswa
C. alikabwa
D. alionekana

**39.** Kulingana na makala haya, Bwana Aisee alikuwa
A. jangili
B. jambazi
C. mkwepuzi
D. tapeli

**40.** Kichwa mwafaka kwa makala haya ni
A. Wajinga ndio waliwao.
B. Akili nyingi huondoa maarifa.
C. Aliye juu mgojee chini.
D. Mbio za sakafuni huishia ukingoni.

*Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali* **41 – 50**

**Tarakilishi ama kompyuta ni kati ya teknoloji mpya ambayo inatumiwa siku hizi karibu kila mahali mathalani katika kampuni kubwakubwa, benki, masoko makubwa, viwandani, viwanja vya ndege, meli, idara za serikali, vyuo, shuleni na kadhalika. Katika shule za upili, tarakilishi ni somo ambalo linashughulikiwa kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne na hutahiniwa katika mtihani wa kitaifa wa kidato cha nne. Aidha, serikali iko katika harakati za kuwapa vipakatalishi wanafunzi wote wa darasa la kwanza katika shule zote za umma nchini.**

Tarakilishi imegawanyika katika sehemu mbili muhimu; programu mfumo na maunzi. Maunzi ni neno jumlishi ambalo hutumika kwa kurejelea vifaa vyote vya kompyuta kwa mfano kichapishi, kishalekezi, kiwambo au skrini, kipanya na mashine chapishi. Programu mfumo ni neno jumlishi ambalo hurejelea programu zote zinazoweza kutumika katika kompyuta.

Vifaa vinavyotumika katika kompyuta ni vingi. Kiwambo hutumika kwa kuonyesha data ambayo inashughulikiwa, nacho kichapishi hutumika katika kuvugulia data hiyo kwa kompyuta. Kishelekezi ni kifaa ambacho huwaka kikizimika kwenye skrini nacho huashiria mahali ambapo data inayovuguliwa itaingia. Pahali pa kishalekezi panaweza kubadilishwa kwa kutumia kipanya. Kipanya ni kidude chenye mkia mithili ya panya. Baada ya kazi kukamilika na data kuwa habari mashine chapishi huichapisha habari hiyo kwenye karatasi ili isomwe na watu wengi iwezekanavyo, pahali pengi na pahali popote.

Tarakilishi ina sifa nyingi muhimu. Chombo hiki kina uwezo wa kufanya hesabu na kazi nyinginezo kwa kasi sana. Sifa nyingine ni kwamba tarakilishi huhifadhi ujumbe mwingi sana kwa matumizi ya baadaye. Maelekezo huchukuliwa na kuwekwa kwa ajili ya kufuatwa na chombo hiki. Mfululizo wa maelekezo haya ndiyo huongoza kompyuta katika wajibu wake na huitwa programu ambayo huandikwa kwa lugha ya kikompyuta. Kompyuta hufuata maelekezo haya kwa kuamshwa na binadamu. Sheria hizi huwa sahili na kompyuta ina uwezo wa kuzitumia ili kufikia uamuzi wa jinsi ya kutenda.

Kuwasiliana na mifumo mingine ya kompyuta ni muhimu sana na kompyuta ina uwezo wa kufanya hivyo. Kompyuta huingizwa data ambayo huchakatwa ili kuleta maana, na uzao wa kuchakatwa huku ndio huitwa habari. Programu ni mfumo wa utaratibu ambao umeandikwa kwa lugha ya kikompyuta. Programu huiwezesha kompyuta kuchakata data na kuifanya iwe habari kwa mfano, inaweza kuongeza nambari mbili au zaidi na kukupa jibu.

Katika kompyuta habari inaweza kuhifadhiwa katika diski ngumu au diski tepetevu. Diski ngumu ni nafasi inayopatikana katika kompyuta yenyewe na inaweza kuhifadhi maktaba nzima. Diski tepetevu ni ile nafasi ambamo disketi huwekwa ili habari inayochakatwa ihifadhiwe kwa disketi. Disketi ni kifaa kidogo mithili ya kaseti. Nafasi hizi za kompyuta zimegawanywa katika viendesha diski kwa mfano ukitaka kuhifadhi habari yako katika diski ngumu, utatumia kiendesha diski A. Ilhali ukitaka kuhifadhi kazi yako katika diski tepetevu utatumia kiendesha diski C.

Kwa hivyo kwa muhtasari, tunaweza kusema kuwa kompyuta ni kifaa au chombo ambacho hufanya kazi kwa kuongozwa na programu iliyohifadhiwa. Kompyuta hujiendesha yenyewe kwa kukubali na kuchakata data ili iwe habari.

41. Kulingana na makala tarakilishi hutumika
A. benkini, viwanjani, shuleni na idara za serikali.
B. benki kubwa, shule zote, viwanjani na sokoni.
C. masoko makubwa, viwanja vya ndege, benkini na vyuoni.
D. mashambani, shuleni, vyuoni na nyanjani.

42. Vipakatalishi vitatolewa kwa wanafunzi
A. wote wa shule za umma.
B. wote wa darasa la kwanza.
C. wa kidato cha kwanza hadi cha nne.
D. wa darasa la kwanza katika shule za umma.

43. Mfano wa maunzi katika kompyuta ni
A. programu, kiwambo, kishalekezi, kipanya.
B. baobonye, mulishi, kipanya, kishalekezi.
C. baobonye, programu, data, disketi ngumu.
D. data, diski, tepelevu, skrini, kipanya.

44. Sehemu kuu za kompyuta kulingana na makala haya ni ngapi?
A. Mbili
B. Tatu
C. Tano
D. Sita

45. Umuhimu wa kompyuta ni kuwa
A. hufanya kazi kwa kasi, huhifadhi ujumbe mwingi.
B. hurahisisha kazi, hutumia nguzu za umeme.
C. huongozwa na programu wala si mwanadamu.
D. ina akili hata kuliko binadamu, ni rahisi kutumia.

46. Sheria hizi huwa sahili, maana yake ni kuwa huwa
A. chache
B. nyingi
C. rahisi
D. ngumu

47. Kulingana na makala haya habari hupatikana baada ya
A. kuhifadhiwa kwenye diski yoyote.
B. data kuingizwa na kuchakatwa.
C. kupelekwa kwa watangazaji.
D. kufikia hadhira iliyolengwa.

48. Watu pia hutumia tarakilishi kuwasiliana kwa njia ya
A. kipepesi
B. simutamba
C. nyaraka
D. barua pepe

49. Lengo la kuchapisha maandishi kwenye karatasi ni kuwa itaweza
A. kusomwa na yeyote.
B. kusomewa mahali popote.
C. kufanyiwa marekebisho.
D. kusomwa kwa vyovyote.

50. Kichwa kifaacho kwa makala haya ni:
A. Sehemu za tarakilishi.
B. Teknolojia ya kisasa.
C. Manufaa ya kompyuta.
D. Jinsi ya kutumia kompyuta.